



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TANGAZO LA MWALIKO WA WATAZAMAJI WA NDANI WA  
UCHAGUZI MDOGO WA MADIWANI KATIKA KATA 23 ZA  
TANZANIA BARA**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uchaguzi mdogo wa Madiwani katika kata 23 za Tanzania Bara. Uchaguzi huo utafanyika siku ya Jumatano tarehe 20 Machi, 2024 katika kata zifuatazo:-

Na.	Mkoa	Halmashauri ya	Kata
1.	Dar es Salaam	Manispaa ya Kigamboni	Kimbiji
2.	Kigoma	Manispaa ya Kigoma/Ujiji	Kasingirima
3.	Tabora	Manispaa ya Tabora	Ndevelwa
4.	Pwani	Mji Kibaha	Msangani
		Wilaya ya Bagamoyo	Fukayosi
		Wilaya ya Kibiti	Mlanzi
5.	Ruvuma	Mji Mbinga	Utiri
		Wilaya ya Songea	Mbingamhalule
6.	Geita	Wilaya ya Mbogwe	Isebya
7.	Lindi	Wilaya ya Kilwa	Kibata
8.	Mara	Wilaya ya Musoma	Mshikamano

Na.	Mkoa	Halmashauri ya	Kata
		Wilaya ya Butiama	Busegwe
9.	Mbeya	Wilaya ya Kyela	Nkokwa
10.	Morogoro	Wilaya ya Mlimba	Kamwene
11.	Mtwara	Wilaya ya Nanyumbu	Chipuputa
12.	Mwanza	Wilaya ya Sengerema	Buzilasoga
		Wilaya ya Kwimba	Mhande
13.	Rukwa	Wilaya ya Nkasi	Kabwe
14.	Simiyu	Wilaya ya Meatu	Bukundi
15.	Tanga	Wilaya ya Muheza	Mkuzi
		Wilaya ya Mkinga	Boma
			Mtimbwani
			Mayomboni

Kwa mujibu wa kanuni ya 16(3) ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za Mwaka 2020, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaalika watazamaji wa uchaguzi wanaotaka kutazama uchaguzi.

Kupitia tangazo hili, Tume inakaribisha maombi kutoka kwa taasisi na asasi mbalimbali nchini ambazo zinahitaji kutazama uchaguzi mdogo katika kata 23 zilizopo katika halmashauri mbalimbali kama zilivyotajwa kwenye Jedwali. Taasisi na asasi zenye nia ya kutazama uchaguzi huo ziwasilishe maombi kwa kutumia anuani (*link*) ifuatayo <https://oms.nec.go.tz>

Barua ya maombi pamoja na mambo mengine itatakiwa kuainisha mambo yafuatayo: -

- i. Anuani kamili ya taasisi au asasi husika;
- ii. Mahali ambapo taasisi au asasi husika inafanyia kazi (Physical address);
- iii. Shughuli ambazo zinafanywa na taasisi au asasi husika kwa mujibu wa hati ya usajili;
- iv. Maeneo ambayo taasisi au asasi inapenda kwenda kutazama uchaguzi;
- v. Idadi ya watu ambao taasisi au asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na majina na taarifa zao binafsi;
- vi. Majina na namba za simu za viongozi wa taasisi au asasi husika kama yalivyoandikwa katika hati za usajili;
- vii. Ikiwa taasisi au asasi inahusisha watendaji wa kimataifa, viongozi wawili ambao taarifa zao zitawasilishwa ni lazima wawe watanzania;
- viii. Kuambatisha nakala au kivuli cha hati ya usajili wa taasisi au asasi husika; na
- ix. Kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika.

**Maombi yatapokelewa kuanzia tarehe 15 hadi 20 Februari, 2024.**

Limetolewa leo tarehe 15 Februari, 2024 na:

  
Kallima, R. K.

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**